# DFID Tanzania

# Mpango wa Kazi 2011-2015

Mei 2011

*Mpango huu utafanyiwa marekebisho kila mwaka*

## Yaliyomo:


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 3 |
| Muktadha | 4 |
| Maono | 5 |
| Matokeo | 7 |
| Uwasilishaji na Rasilimali | 9 |
| Uwasilishaji wa Thamani ya Fedha | 12 |
| Ufuatiliaji na Tathmini | 13 |
| Uwazi | 15 |
| Kiambatanisho 1: Jinsia | 17 |
| Kiambatanisho 2: Muhtasari wa Utaratibu | 19 |

# 1) <u>Utangulizi</u>

Serikali ya Uingereza imedhamiria kupunguza tofauti za fursa tunazoona sasa duniani. Tunaamini kuwa kukuza ustawi wa dunia ni wajibu mwema na ni katika maslahi ya kitaifa ya Uingereza. Misaada ni njia tu, sio suluhisho la kila kitu. Kutengeneza utajiri na maendeleo endelevu ndivyo vitakavyowasaidia watu kujiinua kutoka kwenye lindi la umaskini.

Mwezi Mei 2010, Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa, Andrew Mitchell, aliiagiza tume ya mapitio ya misaada (*Bilateral Aid Review*) kuchunguza kwa makini nchi ambazo Idara ya Serikali ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID) inafanya kazi kupitia programu zetu za moja kwa moja za nchi na kanda. Mapitio haya yalitazama njia bora ambazo Uingereza inaweza kutumia kupambana na umaskini mkubwa, tukihakikisha kuwa tunapata ufanisi mkubwa kabisa kwa kila fedha tunayotumia. Sambamba na hilo, DFID walitathmini ni kwa kiasi gani mashirika ya kimataifa tunayoyapa misaada yanapambana na umaskini.

Tarehe 1 Machi 2011, matokeo muhimu ya mapitio hayo yalitangazwa, pamoja na mabadiliko ambayo misaada ya Uingereza itawaletea watu maskini kabisa duniani katika kipindi cha miaka minne ijayo. Mapitio ya misaada yamebadili kidogo mtazamo wa programu zetu na yametufanya tulenga nchi chache zaidi ili misaada yetu iende pale ambapo italeta tofauti na pale palipo na mahitaji makubwa. Matokeo ya mapitio hayo yanatuwezesha kutoa fedha zaidi kwa mashirika ya kimataifa yenye ufanisi mzuri, ambayo ni muhimu katika kutekeleza vipaumbele vyetu vya maendeleo. Pia, mapitio ya idara inayojitegemea ya misaada ya kibinadamu iliangalia ni kwa jinsi gani Uingereza itaweza kutumia kama msingi uimara wake wa kutoa mahitaji ya kibinadamu na kusaidia kuhakikisha muitikio wa majanga ya baadaye unapangwa na kuratibiwa vizuri zaidi.

DFID imedhamiria kuwa kiongozi wa dunia kwenye uwazi. Katika hali ya sasa ya kifedha, tuna wajibu wa kuonyesha kuwa tunapata thamani kwa kila paundi ya fedha za walipakodi wa Uingereza tunazotumia kwenye maendeleo. Matokeo, uwazi na uwajibikaji ni wito wetu na vinaongoza kila tunachofanya. DFID inaona uwazi ni muhimu katika kuimarisha uwajibikaji wetu kwa wananchi wa Uingereza na kwa wananchi katika nchi tunazofanya kazi. Uwazi utatusaidia pia kupata thamani ya fedha katika programu zetu na itaimarisha ufanisi wa misaada katika jitihada za kupunguza umaskini.

Dhamana ya uwazi wa misaada ya Uingereza inatutaka DFID tuweke misaada yetu wazi kwa wananchi Uingereza na wa nchi zinazoendelea. Kama sehemu ya dhamana hii, tunachapisha Mipango ya Kazi inayoongoza programu zetu katika nchi zote tunakotoa misaada. Mipango Kazi hii inaelezea dira, vipaumbele na matokeo yatakayotolewa katika kila programu yetu ya nchi.

Tutaweka juhudi zetu zaidi katika kusaidia kufikisha Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs), kutengeneza utajiri katika nchi maskini, kuboresha utawala na usalama wao na kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.Tuzo ya kufanya hivyo ni kubwa: maisha bora kwa mamilioni ya watu na dunia salama na yenye ustawi zaidi.

## 2) <u>Muktadha</u>

Tanzania imepata matokeo ya kuvutia ya maendeleo toka mageuzi ya uchumi ya kutoka uchumi uliokuwa ukiendeshwa na serikali kuenda uchumi wa soko huria katika miaka ya 1980 na 1990. Uchumi ulikuwa kwa wastani wa asilimia 7 kwa mwaka tangu 2001 mpaka 2009.

Uwekezaji mkubwa kutoka kwa wahisani umeisaidia Tanzania kupata maendeleo mazuri katika malengo manne kati ya nane ya Malengo ya Milenia ya Maendeleo (Millennium Development Goals - MDGs), na hivyo kuboresha kwa kiasi kikubwa fursa za maisha kwa mtanzania wa kipato cha kati. Karibu watoto wote (wa kiume na wa kike) wameandikishwa katika shule za elimu ya msingi; vifo kutokana na ugonjwa wa malaria vimepungua sana; Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi hayaongezeki na vifo vya watoto vimepungua kwa asilimia 45. Tanzania ina uwezo wa kuwa taifa lenye watu wengi wa kipato cha kati na kuwa kitovu cha biashara katika kanda ya Afrika Mashariki na Kati. Ina utajiri wa maliasili: madini, mafuta, gesi, makaa ya mawe, maji ya maziwa na bahari, na ardhi yenye rutuba. Ni nchi tulivu katika Jumuia ya Afrika Mashariki na ipo katika korido za biashara inayounganisha bandari zake za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga na nchi tano jirani zisizo na bandari.

Kwa bahati mbaya ukuaji mkubwa wa uchumi wa muongo uliopita haujapunguza kwa kiasi kikubwa umaskini wa kipato kwa watanzania wengi. Ukuaji uko tu kwenye sekta zenye mitaji mikubwa kama za madini na mawasiliano, na katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam. Ongezeko la watu – Idadi ya watu nchini Tanzania inatazamiwa kuongezeka kutoka watu milioni 43 na kufikia milioni 75 million mwaka 2030 – linakwenda kwa haraka zaidi kuliko fursa za ajira; chini ya asilimia 10 ya watu wazima wako katika ajira rasmi. Biashara ndogo na zisizo rasmi, ambazo zinasaidia kuongeza mali, zinatatizwa na ukosefu wa mitaji, usafiri duni na umeme usioaminika. Fursa za kutengeneza kipato ni chache, hususan kwa wanawake. Idadi kubwa ya wananchi wanaishi vijijini na wanategemea kilimo cha mashamba madogo madogo ambapo kiasi cha ukuaji na uzalishaji ni kidogo. Wakulima wengi wadogo wadogo wanaathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi na bila ya kuwa na mbegu bora na mbolea, wanahangaika kuzalisha ziada watayoweza kuuza ama hata kulisha familia zao. Wakiwa na bidhaa za kuuza, wanapata shida kupata masoko ya kuuza mazao yao kwa bei nzuri.

Hivyo, ingawa Tanzania si tena moja ya nchi tano maskini zaidi duniani kama ilivyokuwa miaka ya 1980, bado ipo katika nchi 25 maskini zaidi. Asilimia 80 ya watu (watu milioni 34) wanaishi kwa kipato cha chini ya Tsh 40,000 kwa mwezi. Na asilimia 34 ya watu (watu milioni 15) wanaishi kwa kipato cha chini ya Tsh 14,000 kwa mwezi, ikimaananisha kuwa hawawezi kununua bidhaa muhimu kama sabuni na nguo.

Mahitaji ya nchi bado ni makubwa: ni asilimia 34 tu ya watoto wanajiunga na shule za elimu ya sekondari, zaidi ya watu milioni 30 wanatumia huduma za maji taka zisizofaa, asilimia 42 ya watoto wote wanadumaa kwa ajili ya utapiamlo, maliasili zinavunwa kwa kupitiliza, ni moja ya nchi tano duniani yenye vifo vingi vya watu vinavyosababishwa na malaria, na mwanamke mmoja kati ya 25 atakufa kwa ajili ya matatizo wakati wa uzazi. Ukubwa wa nchi, miundombinu duni na idadi ya watu inayoongezeka kwa haraka inaleta changamoto kubwa katika utoaji wa huduma

muhimu kwa usawa nchini kote. Na upanuzi mkubwa wa hivi karibuni katika baadhi ya sekta kama elimu kumemaananisha ubora wa elimu inayotolewa umekuwa ni tatizo kubwa, kama inavyoonekana katika kushuka kwa viwango vya ufaulu wa mitihani ya kumaliza shule. Wanawake na wasichana wana fursa ndogo zaidi ya kumaliza elimu ya sekondari na hawapati huduma ya uzazi wanayohitaji.

Mkakati wa serikali wa kupunguza umaskini unatambua na kushughulikia mambo haya lakini uwezo mdogo wa serikaliunaweza kuleta ugume karika kutimiza malengo haya. Tanzania ni nchi yenye demokrasia changa na uchaguzi mkuu wa 2010 ulikuwa uchaguzi wa nne tu wa vyama vingi katika historia ya nchi baada ya kurudishwa tena mfumo wa vyama vingi. Uchaguzi huo ulionekana kuwa huru na ulionyesha kwamba Tanzania imepiga hatua mbele katika kidemokrasia, hususan kisiwani Zanzibar ambapo serikali ya umoja wa kitaifa unaonyesha dalili za kuvunja urithi wa vurugu za kisiasa. Hata hivyo waangalizi walionyesha mapungufu katika mchakato mzima wa uchaguzi. Ukuaji wa asasi za kiraia umekuwa mkubwa na uhuru wa siasa umedumishwa. Hata hivyo kuna mashaka katika kasi ya utekelezaji wa mageuzi. Kasi imepungua katika maeneo muhimu kama vile mageuzi katika mazingira ya biashara. Rais aliyepo madarakani alikuwa na mwanzo mzuri katika kushughulikia suala la rushwa na Tanzania inazidi kupata mafanikio, lakini bado inapata shida kushughulikia tatizo kubwa la rushwa ndogo ndogo na kuwatia hatiani watuhumiwa wa kesi za rushwa kubwa.

Wahisani na wabia wengine wa maendeleo watahitaji kufanya kazi pamoja kuisaidia Tanzania kufikia uwezo ilionao. Tanzania inabaki tegemezi: misaasa toka kwa wahisani inategemewa kufidia asilimia 30 ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2010/11. Kuna wahisani zaidi ya 40 katika sekta mbalimbali kama vile Benki ya Dunia, asasi za kiraia na wahisani wanaochipukia kama China, India na Brazil. Uingereza imekuwa mmoja wa wahisani wakubwa wa Tanzania na chini ya Mpango Kazi huu tutaendelea wajibu wetu wa uongozi, tukifanya kazi kwa nguvu zaidi kuhakikisha kuwa misaada yote Tanzania ni ya ufanisi kadri inavyowezekana.

# 3) <u>Maono</u>

## Kwa Ujumla

Malengo makuu ya DFID Tanzania ni kuiona Tanzania inapunguza umaskini wa watu wake na kujitegemea. Hii itahitaji mabadiliko yatakayoleta ukuaji endelevu wa uchumi utakaotoa fursa zaidi za ajira na kuinua vipato vya watu wa vijijini. Kwa hiyo mpango wa DFID wa miaka minne ijayo utaongeza nguvu katika sekta binafsi na mfumo wa masoko ili ziweze kutimiza wajibu muhimu wa kupambana na umaskini wa vijijini kupitia ushindani mkubwa, uwekezaji na ushirikiano wa kikanda. Misaada yetu itachangia katika uwekezaji wa umma unaohitajika ili kufanya ukuaji wa uchumi uwe wa pamoja zaidi na wa usawa. Na programu ya DFID italinda mafanikio haya kwa kuisaidia serikali kufanya kazi bora zaidi kwa ajili ya watu wake. Mpango Kazi huu unafungamana na malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa serikali ya Tanzania, MKUKUTA (2010/11 mpaka 2014/15).

Mpango Kazi huu una malengo makuu matatu:

1. **Utengenezaji Utajiri.** DFID itaongeza programu zitakazo inua vipato vya watu maskini vijijini, zitakazo ongeza upatikanaji wa mitaji, zitakazo imarisha unyumbukaji kwa mabadiliko ya tabia nchi, na zitakazo punguza gharama za kufanya biashara. Pia katika programu yetu ya ushirikiano wa kikanda, tutaimarisha juhudi za kupunguza gharama za biashara na usafiri ambazo zinapunguza ushindani wa bidhaa za Tanzania zinazouzwa nje.

2. **Uwasilishaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia.** DFID itatumia kama msingi mafanikio ambayo yamesha patikana katika utoaji wa huduma muhimu kwa jamii, kama vile elimu. Tutashughulikia zaidi maeneo muhimu ambayo serikali ya Tanzania haiwezi kukidhi mahitaji ya watu masikini na walio pembezoni, tukijikita zaidi katika maeneo tuliyo na uwezo na ufanisi.

3. **Kuishinikiza serikali kufanya kazi bora zaidi na kuwasaidia watanzania kuiwajibisha serikali yao.** DFID itasaidia kujenga dola ya kidemokrasia zaidi, inayowajibika na inayoshughulikia mahitaji ya watu wake na kuwasaidia wananchi wa Tanzania kupata na kutumia taarifa za huduma, maslahi na haki zao.

## Mfungamano na vipaumbele vya DFID na serikali ya Uingereza

Zaidi ya kupunguza umaskini, shauku ya Uingereza ni kuimarisha ubia wa kidemokrasia nchini Tanzania, kuwezesha sekta binafsi kuwa imara, na kuhakikisha kuwa Tanzania inabaki kuwa nguzo ya utulivu katika kanda ya Afrika Mashariki na Kati, ikitekeleza wajibu wake katika juhudi za kupambana na uharamia katika bahari ya Hindi. Serikali ya Uingereza pia ina shauku kuisaidia Tanzania kupata ufundi na ujuzi na kuvutia uwekezaji, ikiwemo kutoka Uingereza, kutumia nafasi yake ya kijiografia na utajiri wake wa maliasili – ikiwemo mafuta na gesi. DFID itafanya kazi pamoja na ubalozi wa Uingereza na sekta binafsi kuimarisha mazingira ya biashara na kuimarisha uwezo wa Tanzania kustawi katika uchumi wa kanda na dunia. Kupitia mchango wake katika programu ya Tanzania ya TradeMark East Africa, DFID itasaidia kuwasilisha juhudi za Uingereza za kutekeleza mpango wa biashara huru barani Afrika.

Mpango Kazi huu umefungamana na uwasilishaji wa mageuzi ya mfumo wa vipaumbele vya DFID. Wanawake na wasichana ni muhimu katika mpango huu. DFID itawasaidia wasichana wengi zaidi kumaliza elimu ya sekondari, itawapa wanawake wengi zaidi uhuru wa kuchagua kupata ujauzito, itawahamasisha wanawake kuwa viongozi wa jamii, wakulima na wajasiriamali (angalia kiambatanisho cha jinsia kwa maelezo zaidi).

Kipaumbele cha pili cha DFID ni mabadiliko ya tabia nchi; Mpango Kazi huu unatambua hatari na fursa za mabadiliko ya tabia nchi kwa maendeleo ya Tanzania. Mwaka 2010 DFID ilikamilisha mapitio ya programu ya tabia nchi ambayo ilisaidia kuweka pamoja na kuweka vipaumbele msaada wetu katika eneo hili. Mtazamo wa kuingia kwetu katika mabadiliko ya tabia nchi utakuwa kuisaidia Tanzania kupata fedha za tabia nchi – ikiwemo misaada iliyopo kutoka katika Mfuko wa Kimataifa wa

Tabia Nchi – na kuhakikisha ufanisi katika utoaji wa miradi kupitia serikali, sekta binafsi na asasi za kiraia.

### Nini Tutaacha Kufanya

DFID Tanzania itapunguza kutumia mfumo wa kupitisha msaada kwenye bajeti ya serikali (General Budget Support), kama tathmini ya programu ya nchi ya mwaka 2010 ilivyoshauri. Tathmini hii ilionyesha kuwa katika hali ya sasa kupitisha msaada kwenye bajeti ya serikali si njia yenye ufanisi zaidi ya kuwasilisha matokeo ya misaada yetu na ilipendekeza tupunguze matumizi ya mfumo huo.

## 4) Matokeo

DFID Tanzania italeta matokeo kwa yafuatayo, ikifanya kazi na serikali ya Tanzania na wabia wengine. Matokeo haya yote yatatokana na mchango wa DFID.

| Nguzo/ Kipaumbele cha kimkakati | Ishara | Matokeo yanayotarajiwa |
|---|---|---|
| Kutengeneza Utajiri | Kuinuka kwa vipato vya wanaume na wanawake vijijini. | Watu 563,500 katika miaka minne (asilimia 50 wanawake) |
| Kutengeneza Utajiri | Ongezeko la waty wanaopata huduma za kifedha | Watu 741,000 katika miaka minne (asilimia 75 wanawake) |
| Maji safi na Majitaka | Watu wa vijijini kupata vyanzo vya maji vilivyoboreshwa | Watu 405,000 katika miaka minne |
| Elimu | Watoto wanaosaidiwa na DFID katika elimu ya msingi na sekondari ya chini | Watoto 400,000 kila mwaka kwa miaka minne (asilimia 50% wasichana) |
| Afya | Bidhaa za uzazi wa mpango kupatikana kwa wanawake wa Tanzania na kuwapa uhuru wa kuchagua kupata ujauzito | Wanawake 443,000 kila mwaka wana uhuru wa kuchagua kupata ujauzito |
| Afya | Watoto wa chini ya miaka miwili wanaopata nyongeza za lishe zinazoweza kunyunyuziwa kwenye chakula kuzuia utapiamlo na hatari zinazoambatana nao | Watoto 600,000 kila mwaka mnamo mwaka 2014 |
| Mabadiliko ya Tabia nchi | Idadi ya watu wanaoweza kukabili vizuri athari za mabadiliko ya tabia nchi | Watu 650,000 katika miaka minne |
| Utawala | Wanaume na wanawake wanaoweza kupata taarifa za huduma, maslahi na haki zao | Watu millioni nne katika miaka minne (asilimia 50 wanawake) |

## Ushahidi Unaounga Mkono Matokeo

Kuna ushahidi mkubwa juu ya Tanzania unaotoa picha ya asili ya umaskini na vikwazo kwa ukuaji uchumi jumuishi. Ushahidi unaonyesha kuwa umaskini wa kipato umepungua kidogo tu katika muongo uliopita licha ya ukuaji mkubwa wa uchumi. Wakati huduma za jamii zimepanuka katika sekta ya afya na elimu, ubora wa huduma hizo umebaki kuwa ni tatizo na hazisambazwi na kupatikana kwa usawa, hususan kwa wanaume na wanawake. Ushahidi mkubwa unaotumiwa na Mpango Kazi huu unatoka katika vyanzo vikuu sita:

1. Takwimu rasmi za utafiti wa maendeleo ya kaya na mfumo wa taarifa za uongozi, haswa: Utafiti wa Bajeti za Kaya wa 2007 kwa takwimu za umaskini wa kipato, Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya ya mwaka 2009/10 kwa takwimu za afya, na Mifumo ya Usimamizi wa Taarifa za Elimu na Afya kwa utoaji wa huduma za serikali.
2. Mapitio ya maendeleo chini ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (Mkukuta) wa mwaka 2005 – 2010 yaliyofanywa na serikali na watafiti wa nje.
3. Utafiti wa DFID, ukijumuisha ule wa mabadiliko ya tabia nchi (2010), ukuaji wa uchumi ukilenga watu maskini kwa mtazamo wa jinsia (2011), na uchambuzi wetu wa utawala bora wa nchi (2010).
4. Tathmini ya Programu ya DFID Tanzania (2010), uliotoa ushahidi wa kujitegemea juu ya matumizi ya mfumo wa kupitisha msaada kwenye bajeti na matokeo yanayopatikana.
5. Utafiti mwingine na uchanganuzi kutoka katika vyanzo vinavyojitegemea vya Tanzania kama vile Taasisi ya Afya ya Ifakara, ambayo ni taasisi ya utafiti wa afya inayoheshimika Tanzania.
6. Ushahidi kutoka katika filamu iitwayo “Village Voices,” iliyofadhiliwa na DFID ya inayoangalia maendeleo katika jitihada za kupunguza umaskini katika vijiji vya mbali kati ya mwaka 2005 na 2009.

Ushahidi huu ni msingi wa programu yote ya DFID Tanzania na unatoa msingi imara wa uhakiki wa mahitaji na usimamizi. Hata hivyo, ili kujua matokeo yanayotarajiwa, tumechukua vyanzo vingine vya ushahidi. DFID imefanya uchanganuzi maalumu wa mahitaji na gharama juu ya, kwa mfano utoaji wa bidhaa za uzazi mwa mpango na ujenzi wa vyoo mashuleni. Tumetumia vile vile uzoefu wetu wa nyuma katika programu kama hizi, kwa mfano, katika kuongeza programu za kusaidia asasi za kiraia. DFID imetumia taarifa katika programu za sekta mbali mbali zilizopangwa vizuri na kutekelezwa na wabia, kwa mfano kwenye sekta ya maji na shule za sekondari. Na mwisho tumetumia malengo ya taifa katika maeneo ambayo msaada wetu wa bajeti ya serikali utachangia, kama vile uandikishaji wa wanafunzi mashuleni na kutoa wakunga wenye ujuzi.

Matokeo yanayotazamiwa yanaonekana ni halisi kwa sababu misaada imepangwa kwa uangalifu kuendana na ushahidi wa mahitaji na ufanisi. Katika masuala machache ambapo mapendekezo yanajumuisha maeneo mapya ya kazi (kama vile utoaji wa virutubishi vya lishe vya kunyunyiza vinavyoweza kuongezwa kwenye chakula cha watoto wenye umri wa chini ya miaka miwili) haiepukiki kwamba makadirio ya matokeo yanayotarajiwa ni dhaifu na yatahitaji tathmini ya undani zaidi.

Pale ambapo matokeo yanayotarajiwa yatategemea mambo nje ya uwezo wetu, kama vile ukubwa wa bajeti nzima ya serikali ya Tanzania au kiwango cha ubadilishaji wa Paundi, njia yenye hadhari zaidi imetumika kukadiria matokeo.

### Mantiki ya Thamani ya Fedha

Tathmini ya mwaka 2010 ya programu ya DFID Tanzania ilisaidia sana kujua ngazi za juu za vipaumbele kwa i) kutoa ushahidi mzuri wa thamani ya fedha ya uwekezaji uliopita na ii) kutambua uhitaji wa kuongeza msaada kwenye utafutaji utajiri endelevu kupitia sekta binafsi – ambayo ni kiongozi katika kukuza utajiri – ili kupata matokeo mazuri na thamani ya fedha. Hivyo, misaada iliyopendekezwa inajumuisha kuimarisha na kuongeza njia za mafanikio zitakazotupa thamani ya fedha katika kiwango cha hatari kinachokubalika, na programu mpya zitakazochukua uzoefu kutoka katika programu za majaribio na utendaji bora wa kimataifa kuhakikisha tunapata thamani ya fedha. Kwa mfano, misaada iliyopangwa ya kuongeza utajiri itatengenezwa ili kuchochea uwekezaji mwingi zaidi katika sekta binafsi na hivyo kufanya msaada wetu kuwa na matokeo mengi zaidi, wakati huo huo tukishirikiana na sekta binafsi kubeba hasara zinazoweza kutokea na kuchochea uendelevu wa matokeo yapatikanayo.

DFID itaendelea kufanya kazi kupitia serikali kama ni njia iliyohakikishwa kuwa na thamani ya fedha katika utoaji wa huduma, ikilenga kwenye maeneo ambapo ushahidi unaonyesha uwezekano wa kupata maendeleo ya maana – kama afya, elimu na maji – ikitoa matokeo yaliyotarajiwa kwa gharama nafuu. Gharama ya kitu kimoja kimoja kwa programu nzima zimechambuliwa na zinalingana na za nchi nyingine katika kanda. Pale ambapo hazilingani, kuna maelezo mazuri – kwa mfano ukubwa wa nchi na idadi ya watu. Tutafuatilia gharama za kitu kimoja kimoja kama sehemu ya kusimamia mfumo wa matokeo yetu ya jumla kuhakikisha kuwa hayaongezeki na kukusanya ushahidi wa kuelezea upangaji wa mbele na tathmini.

## 5) <u>Uwasilishaji na Rasilimali</u>

Mpango Kazi huu unaweka usawa katika mifumo tofauti inayotumiwa na DFID Tanzania kutekeleza programu zake . DFID itaendelea kutoa misaada kupitia mfumo wa kupitisha msaada kwenye bajeti ya serikali ya Tanzania, lakini itaongeza programu inazoziendesha moja kwa moja kwa kufanya kazi na serikali na wabia wengine nje ya serikali, kama asasi za kiraia na sekta binafsi. Mantiki inayotuongoza kwenye uchaguzi wetu wa utoaji ni uelewa wa nini kinafanya kazi na mbia gani atafaa zaidi kufanya kazi tunavyotazamia nchini Tanzania. Mizania hii itakuwa katika mapitio.

DFID nchini Tanzania itafanya kazi zaidi na mashirika yanayojitegemea nje ya serikali. Hii itajumuisha kufanya kazi na makundi ya asasi za kiraia kusaidia watu kudai uwajibikaji mkubwa zaidi kutoka kwa serikali ya Tanzania, na kuwawezesha watu kufurahia haki zao. Kwa mfano, katika sekta ya elimu, DFID itafanya kazi na asasi za kiraia kubadilisha mtazamo kuhusu unyanyasaji wa kijinsia mashuleni.

DFID itaongeza programu zake kwa sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na kutumia fedha kutoa mitaji inayohitajika kuhamasisha uwekezaji na ubunifu wa sekta binafsi – kwa mfano, kutenga fedha ili kuchochea changamoto ya ubunifu katika sekta za nishati na biashara za mazao ya kilimo. Pia, tutatafuta fursa za kuongezea na kuimarisha kazi za Taasisi ya Fedha za Maendeleo ya serikali ya Uingereza (CDC Group) nchini Tanzania.

Wahisani wengi na mashirika mengi ya maendeleo yanafanya kazi nchini Tanzania, na kuleta mazingira ya kusongamana ambapo uratibu mzuri ni muhimu. DFID itajenga ubia na wahisani mbalimbali na kuiongoza jumuia ya wahisani kuhakikisha kuna mgawanyo wa kazi wa maana na kuwashinikiza wengine ili kuongeza manufaa ya misaada yetu. DFID itafanya kazi kwa karibu na wahisani wa bajeti ya serikali ili kuongeza uwazi na uwajibikaji. Tutatumia mchanganuo wa mapitio ya misaada ya DFID kuona hatari zilizopo na kuhakikisha tunapata ufanisi mzuri kwa kufanya kazi na wabia mbalimbali. Tukishirikiana na wabia wetu wote na katika programu zetu zote tutafuatilia hatari zilizopo kwa ukaribu na tutafanya tathmini za kibiashara katika michakato ya manunuzi, kupata kinaganaga gharama za kila kitu. DFID pia itatengeneza makubaliano ya mikataba na wabia ili kupata uwazi zaidi katika utendaji na kuripoti matokeo.

DFID itafanya kazi na, ama kupitia, serikali ya Tanzania pale ambapo lengo ni kuimarisha utoaji wa huduma muhimu za kijamii nchini kote. Mifano ya njia hii ni kama kupeleka misaada moja kwa moja katika sekta au kuipitisha kwenye bajeti ya serikali, haswa kwenye maeneo yenye ushahidi kuwa serikali inafanya kazi inavyotegemewa. Hatahivyo, kama kuna masuala magumu haswa yanayohitaji kushughulikiwa, tunaweza kutoa fedha na ujuzi kwa shughuli zilizolengwa, tukishirikiana na wabia wengine. Kwa mfano, Tanzania inapata shida kuhakikisha watoto wengi wanaingia shule za sekondari na kumaliza elimu hiyo. Hivyo, DFID inapanga kutoa fedha zaidi kwa ajili ya Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari ya Tanzania kwa ushirikiano na Benki ya Dunia ili kupanua na kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari haswa kwa wasichana.

Mpango Kazi huu unajumuisha pia msaada kwa serikali ya Tanzania kuimarisha jinsi inavyotekeleza majukumu yake muhimu, kwa sababu hii hatimaye itaimarisha ufanisi na thamani ya fedha ya kila kitu serikali inachofanya. Msaada huu utahusisha zaidi programu zilizolengwa – hasa ndogo ndogo lakini zilizo na matokeo makubwa. Mfano ya njia hii ya kufanya kazi ni pamoja na msaada kwa Shirika la Takwimu la Taifa (*National Bureau of Statistics* ama kwa ufupi *NBS*). Mshauri wa takwimu wa DFID atafanya kazi moja kwa moja na NBS kuimarisha uwezo wake wa kukusanya takwimu zenye ubora kuhusu matokeo.

DFID inasaidia njia za ubunifu na uvumbuzi kwenye ufanyaji kazi, ikitambua kuwa mifumo ya serikali mara nyingine si mizuri sana katika kutoa huduma muhimu. Sekta ya maji ya Tanzania ni mfano mzuri: katika programu ya usambazaji maji vijijini ambayo DFID inapendekeza kugharamia, makundi ya wanajamii watajenga na kusimamia usambazaji wa maji katika jamii zao. Msaada huu utawasaidia haswa wanawake ambao kawaida hutumia mpaka masaa tano wakitembea kutafuta maji katika kipindi cha kiangazi. Katika miaka minne ya Mpango Kazi huu, DFID itajaribu na kutathmini njia mpya za kufanya kazi kwa ufanisi zaidi nchini Tanzania.

**Matumizi ya Programu**

| Nguzo/ Kipaumbele cha Kimkakati | 2010/11 | | 2011/12 | | 2012/13 | | 2013/14 | | 2014/15 | | JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Rasilimali £'000 | Mtaji £'000 | Rasilimali £'000 | Mtaji £'000 | Rasilimali £'000 | Mtaji £'000 | Rasilimali £'000 | Mtaji £'000 | Rasilimali £'000 | Mtaji £'000 | Rasilimali £'000 | Mtaji £'000 |
| Utengenezaji Utajiri | 45,503 | | 43,000 | | 40,000 | | 42,000 | | 42,000 | | 167,000 | |
| Mabadiliko ya tabia nchi | 936 | | 2,000 | | 3,000 | | 3,000 | | 2,000 | | 10,000 | |
| Utawala na Usalama | 41,964 | | 36,000 | | 34,000 | | 32,000 | | 35,000 | | 137,000 | |
| Elimu | 25,982 | | 47,000 | | 57,000 | | 59,000 | | 59,000 | | 222,000 | |
| Afya ya uzazi, kinamama na watoto wachanga | 6,500 | | 2,000 | | 2,000 | | 2,000 | | 2,000 | | 8,000 | |
| Malaria | 0 | | 3,000 | | 4,000 | | 3,000 | | 3,000 | | 13,000 | |
| Afya nyingine | 15,260 | | 9,000 | | 10,000 | | 10,000 | | 10,000 | | 39,000 | |
| Maji safi na Majitaka | 6,566 | | 6,000 | | 8,000 | | 12,000 | | 13,000 | | 39,000 | |
| Umaskini, Njaa na Mazingira magumu | 3,105 | | 2,000 | | 2,000 | | 2,000 | | 2,000 | | 8,000 | |
| Misaada ya kibinadamu | 4,000 | | | | | | | | | | | |
| Jumla Kuu | 149,815 | | 150,000 | 0 | 160,000 | 0 | 165,000 | 0 | 168,000 | 0 | 643,000 | 0 |

# 6) Uwasilishaji na Thamani ya Fedha

## Changamoto

Programu za DFID Tanzania zimekuwa zikitoa thamani nzuri ya fedha (*Value for Money*) , zikitekeleza kazi inavyopaswa wakati huo huo zikiweka gharama za usimamizi chini, kwa asilimia 1.8 ya programu nzima. Hata hivyo kadri programu zinavyobadilika kufuatia mazingira tofauti nchini Tanzania, kuna changamoto mpya za kupata thamani ya fedha katika maeneo yote ya matumizi yetu. DFID inaongeza kwa kiasi kikubwa idadi ya programu inazosimamia Tanzania, hivyo tutahitaji kujenga kanuni za kupata thamani ya fedha katika eneo hili la kazi. Pia tunataka kuhakikisha kwamba thamani tunayopata kutoka katika programu zetu zinazotekelezwa na serikali zinaimarika. Na kadri programu na wafanyakazi watakavyo badilika katika utekelezaji wa mpango huu, DFID itahakikisha inadumisha thamani ya fedha. Vitu tukakavyo fanya kudumisha ufanisi wa gharama za utekelezaji zinaonyeshwa katika sehemu ya 6.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, tutatumia mikakati na dhana za kampuni za kuboresha matumizi ya fedha ili kuhakikisha kwamba tuna mifumo sahihi na utaratibu wa kutuwezesha kuendelea kuboresha usimamizi wa fedha zetu. Tutatengeneza mkakati mpya wa thamani ya fedha na mpango kazi mwishoni mwa mwezi April 2011 kuhakikisha tuna utaratibu mzuri wa kuendeleza uimarishaji wa thamani ya fedha. Mpango huu utazingatia maeneo yafuatayo.

## Uimarishaji wa thamani ya fedha katika programu za DFID

DFID Tanzania itaimarisha uwezo wake wa kushughulikia masuala ya thamani ya fedha katika utengenezaji na utekelezaji wa programu zake zinazopanuka. Tutajenga uelewa wa wafanyakazi wetu na uwezo wao wa kutekeleza mpango kazi wa thamani ya fedha. Mshauri mpya wa thamani ya fedha atatoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wote na atafanya kazi kwa karibu na washauri na wafanyakazi wa miradi. DFID itainua uelewa wa mkakati mpya wa thamani ya fedha katika kazi zetu na wabia – wahisani wengine, mashirika ya kimataifa na asasi za kiraia – ili kupata fursa za kupunguza gharama na kushinikiza kupata matokeo mazuri. Mwisho itaimarisha mifumo na utaratibu ili:

- Kujenga mapendekezo ya thamani ya fedha katika matayarisho ya programu mpya, ikiwamo vipimo vya thamani ya fedha kama vile gharama za kitu kimoja kimoja;
- Kuanzisha utaratibu wa kusimamia thamani kwa mtazamo wa thamani ya fedha;
- Mapitio ya kila mara ya *logframe* na viashiria kuhakikisha usimamizi wa vipimo vya thamani ya fedha na pale inapowezekana kuwa na vipimo vipya na/ama vilivyoimarishwa;
- Kusimamia vipimo kwa kulinganisha na makadirio ya awali na vilinganishi vinavyofaa.

### Uimarishaji wa thamani ya fedha katika msaada unaopitia kwenye bajeti ya serikali ya Tanzania

DFID itaongeza uwezo wa serikali ya Tanzania kuchanganua thamani ya fedha ya matumizi yake kwa kuimarisha ukusanyaji wa takwimu katika utendaji na matokeo. Pia tutaunga mkono mapitio ya pamoja ya matumizi ya fedha za umma ambayo ni njia ya kuchanganua ufanisi wa matumizi ya serikali ya Tanzania. Kama sehemu ya msaada huu, DFID itaendelea kuwaazima timu ya uchumi ya Benki ya Dunia wafanyakazi wetu, na kutumia nafasi yetu kama makamu mwenyekiti wa kikundi kazi cha Wahisani na serikali ya Tanzania cha Usimamizi wa Fedha za Umma kuchochea mageuzi zaidi katika usimamizi wa fedha za umma. Pia tutachochea nia ya serikali ya kuimarisha thamani ya fedha katika matumizi yake kwa:

- Kuongeza mtazamo wa matokeo katika mjadala wa usaidizi wa bajeti kwa kushirikiana na wahisani wengine;
- Kutilia mkazo matokeo makubwa zaidi katika mfumo wa tathmini ya utendaji wa msaada wa bajeti ;
- Kuisaidia ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa mahesabu ya serikali kuimarisha uwajibikaji wa fedha kwa kufanya ukaguzi wa utendaji wa serikali;
- Kuisaidia miradi na programu za misaada kuongeza uwazi na uwajibikaji, ili wananchi wa Tanzania na wabunge waweze kushinikiza uwajibikaji wa serikali;
- Kufanya kazi na wabia wa maendeleo kutekeleza kanuni zilizokubaliwa za matumizi ya posho kwa watumishi wa serikali, ili kupata thamani bora katika utendaji kupitia mifumo ya serikali.

## 7) <u>Ufuatiliaji na Tathmini</u>

DFID Tanzania itaimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kulingana na mabadiliko ya programu na vipaumbele vipya. Mifumo hii imetengenezwa kuhakikisha tunatoa matokeo yanayotakiwa kama yalivyoelezewa katika Mpango Kazi huu.

### Ufuatiliaji

**Vipi:** Programu zote za DFID zitakuwa na mifumo ya ufuatiliaji ambayo itafuatilia maendeleo katika upatikanaji wa matokeo. Wakati huo huo, DFID itaimarisha zana na ujuzi za mfumo wa Tanzania wa takwimu za taifa ili tuweze (1) kuutumia kupima viashiria vya matokeo vya ngazi ya juu vya nchi nzima na (2) kukusanya takwimu zilizonyumbulishwa kwa jinsia ili kuelewa athari tofauti za programu zetu kwa wanawake na wasichana.
**Nani:** Wafanyakazi wa programu za DFID watatathmini utendaji kulingana na viashiria vilivyoelezewa katika mfumo wa matokeo, wakidumisha majadiliano ya mara kwa mara na yenye changamoto na wabia wetu ili kuwawajibisha, na kufanya ziara kwenye miradi kutathmini maendeleo.
**Lini:** Katika kiwango cha chini kila programu itakuwa inafuatiliwa kila mwaka. Maendeleo kulingana na malengo ya Mpango Kazi huu yatafanyiwa mapitio kila

miezi sita na mapendekezo yatapelekwa kwa Afisa Mkuu wa DFID nchini Tanzania pale ambapo utendaji utahitaji kuimarishwa.
**Nini:** Taarifa za ufuatiliaji zitatumika kuangalia kama programu inafanikiwa na, pale inapobidi, kufikiria upya njia za utendaji. Taarifa hizo zitatumika kujua maeneo ya maendeleo mazuri na hafifu ili hatua za kurekebisha zichukuliwe pale ambapo kasi ya maendeleo inakuwa ndogo.

## Tathmini

Tutatengeneza mkakati wa tathmini mwaka 2011 utakaoonyesha njia bora ya kutathmini programu zetu zote kama sehemu ya Mpango Kazi, ikijumuisha kwa jinsi gani tutawashirikisha moja kwa moja walengwa wa misaada ya Uingereza. Njia hii itabadilika kutegemea aina ya programu, lakini DFID Tanzania inalenga kujenga tabia ya kufanya tathmini ikishirikiana na wabia, na kuwasaidia kuhakikisha tathmini zinapangwa kwa uangalifu, zinafanyika na kutumika.

Asilimia 70 ya matumizi yetu yaliyopangwa yanafanyiwa tathmini ya kujitegemea. Hii ni pamoja na maeneo yote ya kazi mpya na za ubunifu (kwa mfano, programu za majaribio za kutoa msaada kulingana na matokeo zitakazowapa motisha wafanyakazi wa sekta za afya na elimu kwenda maeneo ya vijijini, na programu ya vinyunyuvizi vya virutubisho ili kuimarisha lishe kwa watoto). Wahisani wamepanga kufanya tathmini ya pamoja ya kujitegemea kuangalia matokeo ya misaada inayopita kwenye bajeti ya serikali ya Tanzania, na DFID itachangia na kutumia matokeo yatakayopatikana kwa ajili ya tathmini zetu. Kama sehemu ya mkakati wa tathmini yetu ya jumla tutaangalia kama programu nyingi zaid zinahitaji tathmini zinazojitegemea. DFID Tanzania itaongeza uwezo wetu kutathmini programu. Tutamuajiri mshauri kuisaidia ofisi kuhakikisha kuwa tathmini zote za programu zinafanywa kwa kiwango cha juu, na matokeo yanawasilishwa inavyofaa na tutajenga uwezo wa wafanyakazi wetu wote wa programu kusimamia na kupanga tathmini.

## Kujenga Uwezo wa Wabia

Kwa ujumla, tafiti zote za kitaifa za Tanzania ni za ubora unaokubalika, lakini zinahitaji kuendelea kupata misaada ya kifedha kuziboresha. Takwimu za uchumi na za kila mara zinahitaji kuimarishwa. Makadirio ya idadi ya watu yamepitwa na wakati, kitu ambacho kinaweza kuleta athari katika viashiria vingi kama vile viwango vya uandikishaji shule kwa wanafunzi. Ushiriki wetu katika shirika la takwimu la taifa na mifumo ya kufuatilia umaskini itatusaidia kuona mapungufu na kujenga uimarishaji kwa kadri muda unavyo kwenda. DFID Tanzania itaimarisha mfumo wa shirika la takwimu na kupanua shughuli za ukusanyaji na usambazaji wa takwimu, na vile vile kusaidia sensa ya idadi ya watu na kaya ya mwaka 2012.

DFID pia itajenga uwezo wa ndani wa kufanya tathmini tukiendelea na mkakati wetu wa tathmini. Tutafanya kazi na wabia wanaotekeleza programu zetu, vituo vya utafiti, na watafiti wanaojitegemea kama vile kituo cha Afya cha Ifakara ili waweze kuthathmini utekelezaji wa programu.

# 8) Uwazi

## Utendaji kuhakikisha DFID inatimiza ahadi zake kulingana na Dhamana ya Uwazi wa Misaada ya Uingereza

Uwazi – kufanya taarifa za kina za kazi za maendeleo za Uingereza zipatikane – zitasaidia kufanya misaada ya Uingereza kuwa ya ufanisi zaidi na ni kipaumbele kwa serikali ya Uingereza. DFID Tanzania itatimiza ahadi za Dhamana ya Uwazi wa Misaada ya Uingereza kwa njia zifuatazo:

1) Tutaweka kwenye tovuti ya DFID taarifa za kina za miradi yote mipya na programu:

- Tutaweka motisha kuhakikisha taarifa ni za ubora wa hali ya juu, kwa Kiingereza rahisi na zinatolewa mapema.
- Tutatoa muhtahasari wa miradi yetu kwa Kiswahili ili Watanzania wengi waweze kuisoma.

2) Tutakuza upatikanaji mkubwa wa taarifa kwa watendaji wa ndani ili waweze kuwawajibisha viongozi wao kwa:

- Tutafanya kazi na asasi za kiraia wanaowezesha taarifa za fedha za serikali kupatikana na kuweza kutumika katika ngazi za kitaifa na za chini zaidi.
- Tutasaidia mashirika yanayojitegemea yanayotoa taarifa juu ya huduma za jamii kwa wananchi.
- Tutafanya kazi na asasi za kiraia zinazochochea matumizi mazuri ya vyombo vya habari na teknolojia mpya kwa ajili ya kukusanya na kusambaza taarifa.
- Tutaweka taarifa kuhusu programu zetu kwenye mfumo mpya wa serikali wa Usimamizi wa Misaada ya Tanzania na kuwahimiza wengine wafanye hivyo.

3) Tutatoa fursa kwa walengwa wa miradi yetu kutoa taarifa kwa:

- Kuhakikisha taarifa za walengwa zinakusanywa katika mapitio na tathmini za mwaka za miradi.
- Kuhakikisha kuwa taarifa za mrejesho kutoka kwa walengwa zinakusanywa wakati wafanyakazi wanapokwenda kutembelea miradi.

4) Tutawashawishi wabia wetu (serikali ya Tanzania, wahisani wengine na asasi za kiraia) kukuza uwazi katika kazi zao, ikiwemo:

- Kuwataka wabia kuelezea katika mapendekezo yao ya miradi ni kwa jinsi gani watakuza uwazi na kukusanya taarifa za mrejesho kutoka kwa watu wanaofaidika na miradi.
- Kuwashawishi wabia wetu wa utekelezaji kuanza ama kuendelea kutafuta taarifa za mrejesho kutoka kwa wananchi wa Tanzania (kwa mfano taarifa za Mapitio ya Maoni ya Walipakodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, na tafiti ya Maoni ya Watu ya serikali ya Tanzania).

- Kuisaidia serikali ya Tanzania katika ahadi yake ya kuhakikisha kuwa taarifa za fedha zinapatikana na kutumika na watanzania wengi (kwa mfano kwa kutengeneza machapisho ya bajeti ya serikali ambayo ni rahisi kwa mtu wa kawaida kuelewa).
- Kushawishi wizara mbali mbali kuweka taarifa na takwimu muhimu katika tovuti zao. Taarifa hizo ziwe zinapatikana kwa urahisi kwa watu wote (haswa katika sekta za elimu, afya na maji).
- Kushawishi serikali ya Tanzania kupitisha sheria juu ya uhuru wa kupata taarifa.

# Kiambatanisho 1: Jinsia

Tanzania imefanya mageuzi makubwa ya sera na sheria kushughulikia tatizo la tofauti ya jinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana. Jitihada hizi zimeiwezesha Tanzania kupata usawa wa jinsia katika uandikishaji wa watoto kwenye elimu ya msingi, na kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za juu za siasa na serikali, hususan katika utumishi wa umma. Hata hivyo, pamoja na mafanikio haya, wanawake wengi wa Tanzania bado wemebanwa na mifumo ya asili inayowafanya wasipate fursa sawa na wanaume, hasa kwenye viwango vya kipato. wamefungwa katika wajibu za asili za wanawake na wanakuwa wahanga wa ngazi zisizo sawa za kipato. Wanawake nchini Tanzania wanatumia asilimia 14 ya muda wao kila siku kwenye kazi za matunzo (kama kulea, kuhudumia mgonjwa) zisizolipwa; wanafanya kazi kwa masaa mengi zaidi na hawajaelimika kama wanaume. Ukiwalinganisha na wanaume, wanawake wanapata taabu kuweza kumiliki mali kama ardhi na fedha. Wanapata shida kupata huduma kama za afya, wanalipwa kidogo kuliko wanaume na wana ushiriki mdogo katika shughuli za kiuchumi, na kwa hiyo wamefaidika kidogo sana kwenye ukuaji wa uchumi.

Programu yetu ya jinsia imeegemea msingi miwili muhimu: Mchanganuo wa DFID wa Utawala Bora Tanzania, ambao unatathmini mazingira yote kuhusiana na jinsia, na utafiti wa Ukuaji Jumuishi wa Uchumi uliogharamiwa na DFID unaotoa uchanganuzi juu ya ushiriki wa wanawake katika uchumi. Tutatekeleza programu zetu kwa kufanya kazi na wabia wanaofaa katika muktadha tofauti: sekta binafsi kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi wanawake, asasi za kiraia kukuza haki za wanawake na wasichana, na mashirika ya kimataifa ama serikali pale ambapo inaweza kutekeleza programu kubwa nchini kote. Timu ya uhamasishaji ya jinsia, ikitumia uzoefu wa DFID Tanzania katika kutekeleza sera za kijamii na kiutawala, itawajibisha timu nyingine kuelezea utendaji kwa mtazamo wa jinsia.

Wanawake na wasichana ni muhimu sana katika kazi za DFID Tanzania. Programu zetu ama zinawalenga moja kwa moja au zinawapa kipaumbele kama walengwa wakuu wa misaada yetu. Mpango Kazi huu una programu za kimkakati za kuwalenga wanawake na wasichana, ambazo pia zinaambatana na mageuzi ya mfumo wa vipaumbele vya DFID, zitakazotekelezwa katika miaka minne ijayo. Maeneo hayo ni:

**Wasichana kumaliza elimu ya sekondari:** DFID itasaidiana na serikali kusaidia kuongeza idadi ya wasichana wanaomaliza elimu ya msingi na kwenda elimu ya sekondari kwa kuwawezesha wasichana 75,000 kumaliza elimu ya msingi na wengine 40,000 kumaliza elimu ya sekondari. Tutaimarisha ubora wa elimu kwa kufundisha walimu wengi na kuwekeza kwenye miundombinu ya shule ikiwemo ya vyoo na majitaka.

**Kuwezeshwa kiuchumi:** DFID itachochea uwezeshaji kiuchumi wa wanawake kupitia ongezeko la programu zenye mafanikio zinazotoa mafunzo ya ujuzi wa biashara, ushauri, upatikanaji wa masoko, na upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wanawake. Hii ina maana kuwa kupitia programu za DFID, wakulima wanawake 280,000 wataongeza kipato chao na wanawake 560,000 watapata fursa ya kupata mitaji.

**Kushughulikia unyanyasaji dhidi ya wanawake na wasichana:** Unyanyasaji wa kijinsia umeenea nchini Tanzania. Kuna wabia wengi wanaofanya kazi katika eneo hili lakini tatizo la unyanyasaji wa wasichana mashuleni limepewa kipaumbele kidogo sana. DFID itafanya kazi na asasi zisizokuwa za serikali (NGOs) pamoja na serikali kutengeneza mbinu inayofaa ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia shuleni, ikitumia program za majaribio na kuimarisha utetezi katika ngazi zote ili kupunguza kukubalika kwa unyanyasaji wa kijinsia.

**Usambazaji huduma za maji, majitaka na elimusiha:** Ili kuongeza mahudhurio ya wasichana shuleni na kuboresha afya zao, DFID itajenga vyoo 2,500 na karo 250 za kuoshea mikono katika shule za msingi na sekondari. Pia tutashirikiana na serikali ya Tanzania kuwasambazia maji watu 430,000 katika jamii za vijijini ili kupunguza umbali mrefu wanawake na wasichana wanaotembea kutafuta maji.

**Kuongeza uhuru wa kuchagua:** DFID itawapa wanawake 443,000 uhuru wa kuchagua juu ya kupata ujauzito. Hii itaepusha mimba 600,000 zisizotakiwa, utoaji mimba 94,400, vifo vya kina mama 1,880 na vifo vya watoto 34,000.

**Kuwezeshwa kisiasa:** DFID itaongeza ushiriki wa wanawake katika michakato ya kidemokrasia na kisiasa kwa kutoa elimu ya mpigakura kwa wananchi milioni 10 itakayosambazwa kwa vikundi tofauti vya walengwa (wanawake, vijana, n.k), na vile vile kuwawezesha karibu wanawake milioni mbili kupata taarifa juu ya maslahi na haki zao.

**Lishe:** DFID itafanya programu ya majaribio itakayo ongeza virutubisho kwenye chakula vijijini ili kuimarisha afya za kina mama wakati wa kujifungua na kupunguza hatari za kudumaa kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano.

## Kiambatanisho 2: Muhtahasari wa programu zetu

| MSAADA | MAELEZO | £ Million |
|---|---|---|
| **MABADILIKO YA TABIA NCHI** | | **JUMLA: 10** |
| Ubunifu na sekta binafsi | Fedha za changamoto kuchochea ubunifu wa sekta binafsi katika upatikanaji wa nishati safi na kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi katika kilimo | 5 |
| Asasi za kiraia na vyombo vya habari | Kukuza uelewa wa watanzania wa maana za mabadiliko ya tabia nchi na kujenga hamasa ya kukabiliana nayo | 2 |
| Kuimarisha taasisi | Kuimarisha sera za Tanzania na taasisi mbali mbali ili kushughulikia athari za mabadiliko ya tabia nchi kwenye uchumi | 3 |
| **ELIMU** | | **Jumla: 54** |
| Msaada wa fedha kulingana na matokeo | Majaribio kutumia njia ya misaada inayotegemea matokeo ili kuzipa motisha halmashauri za wilaya kutoa wafanyakazi wanaofaa (walimu na manesi) kwenda maeneo ya mbali yasiyofikika kwa urahisi | 2 |
| Msaada kwa programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari | Kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari ya mpaka kidato cha nne ikiwa na mtazamo wa kuimarisha usawa kwa wasichana na wavulana | 44 |
| Maji safi na majitaka mashuleni | Kuimarisha upatikanaji wa maji safi na huduma za majitaka kwa wasichana (na wavulana) mashuleni na kuimarisha elimusiha | 8 |
| Majaribio ya shule salama | Majaribio ya kuimarisha usalama wa wasichana katika mazingira ya shule na kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia mashuleni | Kupitia programu za asasi za kiraia na vyombo vya habari (angalia chini) |
| Utafiti wa Kitaifa wa Kusoma na Kuhesabu (UWEZO) | Kutengeneza takwimu zinazoonyesha uwezo wa watoto wa kusoma, kuandika na kuhesabu kupitia tafiti za kaya zitakazofanywa kila mwaka na asasi zisizokuwa za serikali ili kuinua uelewa wa wananchi na kuwawezesha wazazi kudai elimu ubora zaidi kwa watoto wao. | |
| **UTAWALA NA USALAMA** | | **Jumla: 90** |
| Takwimu nzuri | Kuimarisha upatikanaji na ubora wa takwimu za matokeo zinazotolewa na Shirika la Takwimu, ikiwa ni pamoja na msaada kwa ajili ya sensa. | 8 |
| Asasi za kiraia/ vyombo vya habari | Kusaidia asasi za kiraia na vyombo vya habari kuiwajibisha serikali | 41 |
| Uchaguzi | Kufanya kazi na wahisani wengine na watanzania kwa ajili ya uchaguzi | 6 |
| Usimamizi wa Fedha za Umma | Kuimarisha ubora wa usimamizi wa fedha za umma | 8 |
| Taasisi za kufuatilia/ | Kuimarisha uwezo wa taasisi muhimu za serikali | 27 |

| | | |
|---|---|---|
| Demokrasi | kupambana na rushwa (zikiwemo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, mahakama na polisi) | |
| **AFYA** | | **Jumla: 34** |
| Kupanga familia | Kuwapa wanawake uhuru wa kuchagua na kuimarisha upatikanaji wa uzazi wa mpango kupitia programu za jamii | 8 |
| Takwimu za afya | Kufanya kazi na asasi za kiraia kufuatilia matokeo ya uwekezaji wetu katika huduma za afya | 4 |
| Kuzuia malaria | Kutoa vocha kwa kinamama wajawazito waweze kupata vyandarua ili kujikinga na malaria | 13 |
| Virutubishi vya lishe na mpango wa chakula vijijini | Mpango wa majaribio wa kuimarisha lishe kwa wanawake kwa mtazamo wa kutoa virutubisho muhimu vya lishe kupitia vimfuko vya kunyunyuzia kwa watoto wa umri wa chini ya miaka miwili | 9 |
| **MAJI SAFI NA MAJITAKA** | | **Jumla: 26** |
| Usambazaji maji vijijini | Kusaidia jamii za vijijini kujenga vituo bora vya maji safi wakishirikiana na serikali za mitaa | 16 |
| Usimamizi wa Rasilimali za maji | Kusaidia (huenda tukishirikiana na wizara ya maji ya China) ofisi za serikali za bonde la maji kuweka haki za maji na sera za kusimamia matumizi ya maji | 10 |
| **UTENGENEZAJI UTAJIRI** | | **Jumla: 109** |
| Mfuko wa Changamoto kwa biashara ya kilimo | Kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi na ubunifu katika kuongeza ubora wa bidhaa za kilimo na biashara ya kilimo | 11 |
| Mazingira ya kuwezesha biashara | Kupunguza gharama za kufanya biashara nchini Tanzania, mahsusi kupitia mageuzi ya usimamizi wa kodi, na kurahisisha utoaji wa leseni za biashara | 10 |
| Sekta ya Fedha | Kuongeza upatikanaji wa huduma nafuu na za kufaa za fedha kwa kaya za vijijini na biashara ndogo na za kati | 13 |
| Upatikanaji wa masoko kwa wakulima wadogo | Kuongeza vipato vya watu wa vijijini kwa kuwaunganisha wakulima wadogo na masoko yenye thamani kubwa ya kanda na kimataifa | 21 |
| Trademark Tanzania | Kupunguza vikwazo katika biashara ya kikanda na ushirikiano wa kiuchumi kwa kuongeza ufanisi katika ukanda wa usafiri na ujenzi wa vituo vya forodha mipakani | 24 |
| Mpango wa vocha ya masoko | Mpango wa vocha ya masoko kuongeza upatikanaji wa zana muhimu za kilimo kwa wakulima wadogo (mbolea, mbegu, n.k) zikitolewa kupitia sekta binafsi | 30 |
| **Msaada kwa Bajeti (Kisekta na Jumla)** | **Kuisaidia serikali kutoa elimu, afya na huduma nyingine za msingi** | **Jumla: 320** |
| | | **JUMLA KUU**: **643** |